JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI
TUME YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI

# TAARIFA KWA UMMA

## KUANZA KWA UKAGUZI WA UZINGATIAJI WA SHERIA YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI KWA WAKUSANYAJI NA WACHAKATAJI WA TAARIFA BINAFSI.

**Dodoma – Agosti 28, 2026.**

Katika kuhakikisha kuwa utekelezaji wa matakwa ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Sura ya 44 (PDPA), Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) tayari imeanza zoezi la Ukaguzi wa Uzingatiaji wa matakwa ya Sheria hiyo kwa wakusanyaji na wachakataji wa Taarifa Binafsi Nchini.

Tume ilitoa muda wa kutosha kwa taasisi, mashirika, wafanyabiashara na wadau wote wanaokusanya na kuchakata Taarifa Binafsi kujiandaa na utekelezaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

Kwa sasa Tume inaendelea kufanya ukaguzi wa uzingatiaji unaolenga kuhakikisha kwamba Taarifa Binafsi za watumiaji wa huduma mbalimbali Nchini zinakusanywa, kuchakatwa na kuhifadhiwa kwa kuzingatia matakwa ya Sheria. Ukaguzi huu unajumuisha mambo yafuatayo:-

1. Kuhakiki iwapo taasisi inayokusanya na/au kuchakata Taarifa Binafsi imesajiliwa na Tume kwa mujibu wa Kifungu cha 14(1) na 14(2) vya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Sura ya 44;

2. Kuhakiki usahihi wa Taarifa za usajili zilizowasilishwa na wakusanyaji na wachakataji wa Taarifa Binafsi kwenye rejesta ya Tume;

3. Kuhakiki utekelezaji wa majukumu ya Afisa Ulinzi wa Taarifa;

4. Kuhakiki namna Taarifa Binafsi zinavyokusanywa, kuchakatwa, na kuhifadhiwa;



Mtaa wa Moshi 1, Viwandani, S. L.P 1105, 41102 Dodoma - Tanzania
Simu: +255718462536, +255744057652, +255736110505.
@pdpc.tz @pdpc_tz www.pdpc.go.tz

# TAARIFA KWA UMMA

5. Kuhakiki usalama wa Taarifa Binafsi dhidi ya upotevu, uteketezaji, ubadilishaji, upatikanaji au uchakataji wa taarifa bila idhini kwa mujibu wa Kifungu cha 27(1) cha Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binasi Sura ya 44;

6. Kuhakiki utaratibu wa usafirishaji wa Taarifa Binafsi nje ya nchi kama inavyoelekezwa kwenye Kifungu cha 31 na Kifungu cha 32 cha Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Sura ya 44; na

7. Kuchukua hatua za kisheria ikiwemo kutoa adhabu na faini kwa wakusanyaji na wachakataji wa Taarifa Binafsi wasiozingatia matakwa ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Sura ya 44.

Tume inatoa wito kwa wakusanyaji na wachakataji wa Taarifa Binafsi kuhakikisha kuwa:-

1. Wamesajiliwa katika rejesta ya Tume;
2. Wanazingatia haki za wahusika wa Taarifa;
3. Wanakusanya na kuchakata Taarifa Binafsi kwa madhumuni halali na mahususi yaliyokusudiwa;
4. Wanawasilisha Ripoti ya Uzingatiaji Kila Robo ya Mwaka;
5. Wanazingatia Sera ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi iliyoidhinishwa na Tume;
6. Taarifa binafsi hazisafirishwi nje ya mipaka ya nchi kinyume cha Sheria; na
7. Wanapata ridhaa ya wahusika wa Taarifa kabla ya kukusanya na/au kuchakata Taarifa zao Binafsi, pale inapohitajika.

Tume inautaarifu umma kuwa zoezi la ukaguzi kwa hatua inayofuata litahusisha kutembelea wakusanyaji na wachakataji wa Taarifa Binafsi ili kuendelea kujiridhisha na uzingatiaji wa matakwa ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sura ya 44. Tume inategemea ushirikiano kutoka kwa wadau wote katika kufanikisha zoezi hili.

Kwa taarifa zaidi tembelea tovuti yetu www.pdpc.go.tz au wasiliana nasi kwa namba za simu +255753459155 +25571846253; +255744057652; +255695507751; na barua pepe helpdesk@pdpc.go.tz

**Imetolewa na:**
**Dkt. Emmanuel Lameck Mkilia**
**Mkurugenzi Mkuu - PDPC**



Mtaa wa Moshi 1, Viwandani, S. L.P 1105, 41102 Dodoma - Tanzania
Simu: +255718462536, +255744057652, +255736110505.
@pdpc.tz @pdpc_tz www.pdpc.go.tz